

Jina:

Nambari:

Sahihi:

Tarehe:

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Lugha

Julai/Agosti 2014

Muda : saa 2½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA WILA YA TRANS -MARA MAGHARABI

Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Lugha

Julai/Agosti-2014

Muda : saa 2 ½

MAAGIZO

- Andika **jina lako** na **nambari yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali **yote**. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. UFAHAMU.

Soma makala yafutayo kisha ujibu maswali.

Ingawa wenye hekima walisema macho hayana pazia, ni muhimu kuyatumia macho ulivyojaliwa na muumba wako. Ndio maana ninaamini pia kuwa macho hayafilisi duka!

Mimi hupenda kuyafumbua macho pima kila nitembeapo barabarani au hata ninapokaa nyumbani kusakura yalio karibu nami. Lakini, kuna matukio ambayo hunisumbua na kunisikitisha. Hunisumbua kwa sababu sipati majibu kwayo; hunisikitisha kwa sababu ya athari zake na mihemko yanayoleta katika hisia zangu za ndani. Kila mara hujiuliza; “Kwa nini watu wengi huteseka namna hii duniani? Kwa nini mtu adamke mafungulia ng’ombe akielekea kibarua kila siku bila kusita huku wachache wakistarehe? Kwa nini ugonjwa unaweza kumvamia mtu ghafla bin vuu na kumlemaza ama kumtaabisha kwa muda mrefu kabla ya kumuua? Kwa nini? Mbona kila mtu anapokuwa akisikitika, kuna mwenzake huwa anacheka? Ama maisha ni kitendawili tu?

Hata hivyo, Linalonishangaza sana wakati mwingine ni jinsi wale ninaowafikiria kuwa wanataabika wanavyochukulia hali zao. Utawaona akina yahe wakitabasamu kila mara na kucheka hata matumbo yakiwaguruma. Utawasikia wakiulizana; Umeshindaje?

Hii ndio sababu wakati mwingi moyo wangu huanza kuhisi kuwa labda siku ya kiyama inakaribia zaidi. Wewe hebu fikiria, wanasayansi wanao tuambia kila mara kuwa wamevumbua hiki ama kile ambacho kitafanya maisha ya mwanadamu kuwa rahisi zaidi, ndivyo tunavyojitumbukiza katika majanga na matatizo zaidi maishani. Hii ndio sababu hata ile dhana iliyokuwapo miaka ya nyuma kuwa maradhi ya ukimwi ambayo yamekosa tiba hadi sasa kando na kuwaua mamilioni ya watu, yalitokana na ajali ya kisayansi huko Marekani inaweza kupata masikio.

Swali la kujiuliza ni: “Ni kwa nini maisha yanaposemekana kuwa yamebadilika na kuwa mazuri siku hizi ikilinganishwa na zamani mimi naona kinyume? Au wewe waonaje? Mbona zamani, kabla ya majilio ya kile siku hizi kinaitwa “Maendeleo” watu walikuwa wakitembea tu na kula matunda na mimea, watoto wakicheza na kucheka kwa furaha bila bughudha yoyote? Au hata mbona watu hawakuwa na ubinafsi niuonao siku hizi?”

Maendeleo hayo tunayoyataja kila siku nayaona kama ongezeko la chuki, uhasama, magonjwa, ubinafsi, vita, ufidadi nahujuma dhidi ya mazingira ambamo mwanadamu anafaa kufurahia maisha. Ukweli ni kwamba maendeleo hayo yamepelekea watu wengi zaidi ulimwenguni kuishi katika mitaa ya mabanda, kuwa na nyuso za “sitaki mchezo” na karibu lakini usidowee.”

Ninapozama zaidi katika bahari ya luja kuhusu hali hii duniani ndivyo ninavyochanganyikiwa zaidi kuhusu ukweli halisi. Maajuzi nimeishitakia hali hii kwa Mola ingawa sijajaliwa jibu. Hata hivyo, ninavyoendelea kulingonja jibu ndivyo ninavyoendelea kuelewa ile dhana kuwa ulimwengu ni kokwa ya fuu huishi atamu, anayekwisha ni binadamu.

Maswali.

- (a) Kwa nini mwandishi anadai kuwa labda siku ya kiyama imefika? (al.2)
- (b) Unafikiri ni kwa nini mwandishi anayaona madai kuhusu maendeleo duniani kuwa ni kinaya?
- (c) Mwandishi wa taarifa anamaanisha madai kuhusu maendeleo duniani kuwa ni kinaya. Mwandishi wataarifa anamaanisha ni kwa kusema: (al.3)
 - (i) Kuwa na nyuso za ‘sitaki mchezo’
 - (ii) ‘Karibu lakini usidowee.’

- (d) Yalinganishe maisha ya 'kabla ya maendeleo' na ya sasa ambayo mwandishi anadaini duni kuliko ya zamani. (al.4)
- (e) Eleza maana ya neno na vifungu hivi kama vilivyotumika katika taarifa; (al.4)
- (a) Kusakara
- (b) Macho hayafilisi duka
- (c) Bahari ya luja
- (d) Ulinwengu ni kokwa ya fuu huishi utamu, anayekwisha ni binadamu.

2. MUHTASARI.

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) barani Afrika. Lugha ambazo zimekuwa zikitumiwa ni za kimagharibi kama vile kijerumani, kifaransa na kiingereza. Idadi kubwa ya waafrika, hasa wanaoishi vijijini hawazifahamu lugha hizi.

Uamuzi wa shirika la *Microsoft* wa kutumia lugha ya kiswahili katika *program* za kompyuta kuanzia mwaka 2005 ni mchango mkubwa. Kuzinduliwa kwa mradi huu ni tukio la kipekee kuimarisha teknolojia sehemu za mashambani.

Mradi huu umewawezesha wananchi takribani milioni 150 wa janibu za Afrika Mashariki kufaidika na huduma za tarakilishi.

Utekelezaji wa mradi halikuwa jambo jepesi. Kwanza, ilibidi shirika la *Microsoft* chini ya uongozi wa *Bill Gates* kulishawishi Bodi lake la wakurigenzi. Bodi liliposhawishika kuwa Kiswahili ni lugha inayotumiwa na mamilioni ya watu liliidhinisha kuzinduliwa kwa mradi. Hatua iliyofuatia ilikuwa kuteua maneno 700,000 ya kimsingi ya kiingereza ambayo yangetafsiriwa kwa kiswahili.

Hatua iliyofuata ilikuwa ya kutafuta ushirikiano na dola pamoja na mashirika ya kibiashara na taasisi za elimu ulimwenguni. Ilipobainika kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yangehanasisha Uwekaji katika vituo vya mtandao vijijini, ushirikiano katika kuendesha mradi huu uliafikiwa bila shida. Mradi huu ulichukua muda wa miezi 18 kukamilika. Uliwashirikisha wahisika katika uwanja wa teknolojia ya habari mawasiliano, elimu biashara na idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Africa Mashariki. Vyuo – vikuu ni pamoja na Dar es Salaam, Nairobi, Kenyatta na Makerere.

Waatalamu walioshirikishwa walisaidia katika kubuni faharasa ya istilahi za Kiswahili 3,000. Hizi ni zile ambazo zinafaa kwa matumizi ya kompyuta ya kawaida na ya kila siku.

Mradi huu umeshangiliwa na wakereketwa na wapenzi wa Kiswahili katika nyanja zote. Wasomi, wanariadha, wanamuziki, watalii, wafanyabiashara, wanasiasa, wafuasi wa dini mbalimbali na wakulima; wote wamefurahia hatua ya Kiswahili kuingizwa kwenye mtandao.

Watu ambao walikuwa hawawezi kutumia tarakilishi kwa sababu ya kutojua Kiingereza sasa hawana kisingizio. Matumizi ya kiswahili yatapanua na kuimarisha mawasiliano baina ya watu wanaoishi vijijini na pembe zote za ulimwengu.

Jambo la kutia moyo zaidi ni kuwa sasa vyuo vikuu vinavyotoa masomo kwa kutumia mitandao vimepewa idhini ya kutumia programu hizi. Walimu na wanafunzi wanapata habari moja kwa moja kwa

kiswahili bila kutafsiri . Kuna uwezekano sasa wa kusambaza mafongo katika nyanja na viwango vyote kwa mfumo wa elimu ya mbali.

Katika ulimwengu wa utandawazi tukio kama hili lina manufaa makubwa. Wananchi wa vijijini wanaweza kupata habari na maarifa kutoka pembe zote za dunia na kuhusu masuala tofauti tofauti kwa lugha wanyoielewa barabara.

Kusambaa kwa matumizi ya ngamizi vijijini kutaimarisha biashara inayofungamana na teknolojia na mawasiliano .Haili hii itanua maendeleoya teknolojia na kiwango cha maisha vijijini. Bila shaka mwachano uliopo baina ya sehemu za mijini na vijijini utapunguwa.

Haya ndiyo maendeleo anayokamia kila mja wa siku hizi . Lililopo ni serikali kupania kupanua na kusambaza munda mbinu kama –umeme na simu katika sehemu zote za nchi. Pamoja na haya , kuna haja ya kupunguza bei ya ngamizi na vipuri vyake ili kuwatia motisha watu kununua kompyuta kwa wingi. Ikumbukwe – kuwa lengo la kuanzisha mradi huu ilikuwa kuisaidia serikali kupanua na kusambaza matumizi ya huduma za kompyuta na mtandao katika shule, vituo vya kijami na maeneo ya makaazi. Huduma hizi ni msigi wa elimu, biashara na mawasiliano ya makaazi.

Maswali

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 45-55) (al.6)

(b) Fupisha faida za mradi wa kutumia Kiswahili katika *program* ya kompyuta. (Maneno 45-55) (al.6)

(c) Eleza kwa ufupi serikali inahitaji kufanya nini ili kufanikisha mradi huu? (Maneno 15 -20)

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) ***Tofautisha matumizi ya kiashiria ‘huyu’ katika sentensi hizi.*** (al.2)

(i) Huyu aliajiriwa kazi mapema leo.

.....
.....

(ii) Mkurugenzi huyu amesifika sana.

.....
.....

(b) ***Tambua viambishi awali na tamati katika :*** (al. 3)

Aliyemtorosha

.....
.....

(c) ***Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.*** (al.3)

Mtumishi alifagilia chakula.

.....
.....

(d) ***Unda nomino mbili kutokana na kitenzi hajiri.*** (al.2)

.....
.....
(e) **Huku ukitolea mifano, eleza matumizi mawili ya 'ki'** (al.2)

(i).....

(ii).....

(f) **Jaza pengo.**

Kutenda	kutendewa	Kutendeka
(i) Fumba
(ii) Kaza

(g) **Tamia kirejeshi 'o' kuandika upya sentensi ifuatayo;** (al.2)

Kokoto ambayo alijengea ilifaa.

.....

.....

(h) **Kanusha; Atawafuata kwenda kuukwea mlima.** (al.2)

.....

.....

(i) **Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia "ila"** (al.2)

Rosa alijikamua. Rosa hakuweza kupanda mtini.

.....

.....

(j) **Eleza matumizi ya -ji- katika:** (al.2)

Alijisemea

.....

.....

(k) **Bainisha ,Kirai nomino na Kirai ; kitenzi.** (al.2)

Punde mkongwe ameshindwa kutembea.

.....

.....

(l) **Kanusha ;** (al.2)

Wewe unaitwa ukanywe chai.

.....

.....

(m) **Changanua kwa njia ya jedwali;** (al.2)

Mbuzi mweupe alinunuliwa juzi

.....

.....

(n) **Liandike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.**

"Leo nitachimba mtaro uelekeze maji shambani mwangu" Mkulima alisema.

(al.3)

.....
.....
.....
(o) **Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya ingawa.** (al.2)

.....
.....
(p) **Tambua shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika ;** (al.2)

Idi alimjengea nyumba mpenziwe.

.....
.....
(q) **Isihishe sentensi hii kwa njia tatu tofauti.** (al. 3)

Pale kwao ndiko walimofumaniwa wahalifu.

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
(r) **Onyesha vivumishi katika sentensi ifuatayo na useme ni vya aina gani**
Rinda la msichana limeraruliwa na mvulana mtundu. (al.2)

4. **ISIMU JAMII**

Fafanua maana ya upangaji lugha huku ukieleza majukumu matano yanayoshughulikiwa katika upangaji lugha. (al.10)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com